



JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

Idara ya Zana Za Kilimo na Umwagiliaji

Usindikaji wa Muhogo



**Mashine ya kukereza muhogo kwa kutumia
Injini (Powered Chipper)**

Imetayarishwa na:

Wizara ya Kilimo

Idara ya Zana za Kilimo na Umwagiliaji

S.L.P 2182

DODOMA

UTANGULIZI

MUHOGO ni zao linalotumiwa kwa chakula katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Ni zao pia linalofaa kwa biashara lakini limekuwa likikwamishwa kukua kutokana na mambo mbalimbali yakiwemo masuala ya wakulima kuwa na elimu ndogo ya kulisindika. Ni asilimia 15 tu ya zao hilo husindikwa kwa teknolojia ya asili na bora.

Ili kupata unga bora ni muhimu kuvuna muhogo uliokomaa vizuri ambao haujashambuliwa na magonjwa na wadudu au kuchubuliwa. Muhogo uliovuwa unaweza kuwekwa katika mifuko au maboksi safi na kusindika mapema iwezekanavyo.

Zana za kuvunia muhogo - Jembe la mkono, panga, gunia Ubebaji na Usafirishaji:- Tumia Baiskeli, mkokoteni, trekta au magari

USINDIKAJI KWA KUKEREZA MUHOGO

Kukereza muhogo kunaweza kufanywa kwa kutumia nguvu ya mwanadamu, ingini, mashine za umeme au mashine za nguvu ya upepo. Kunakuwepo na tofauti ya matumizi ya nguvu mbalimbali za mashine. Hii inategemeana na upatikanaji, ubora, uwezo wa kifedha wa mnunuzi, mahitaji kama unga, chips, kiasi cha mali ghafi kilichopo n.k.

VITU VYA KUZINGATIA WAKATI WA KUKEREZA MUHOGO

- Hakikisha kama mashine inatumia mafuta yawe bora
- Lisha mashine sawaswa na mali ghafi bila kupoteza muda kuepuka nguvu na mafuta kupotea bure
- Kuweka kumbukumbu, kama za tarehe, mhudumu(operator), kiasi cha mafuta yaliyotumika
- Makaushio yawe safi na yawekwe mahali pasafi.

HATUA ZA USINDIKAJI

- Saga muhogo uliooshwa na kukaushwa vizuri kwenye mashine ilikupata *chips*. (Chipper)
- Weka muhogo uliokerezwa kwenye vyombo safi
- Anika kwenye vichanja safi
- Peleka kwenye mashine kwa ajili ya kusaga.

- Chekecha kwa kutumia chekeche laini. Ukubwa wa matundu ya chekecheke hutegemea kiwango cha ubora wa unga kinachotakiwa na soko.
- Weka unga kwenye mifuko kutegemea matakwa ya soko (kilo 1, 2,5,10 au 50).

MATUMIZI

Unga bora wa muhogo (HQCF) hutumika kupikia ugali, uji, na katika kutengeneza keki, maandazi, kababu, biskuti, tambi, donate, mkate, chapati n.k.

FAIDA ZA USINDIKAJI

- Muhogo una virutubisho muhimu kwa mwanadamu kama proteini, madini, vitamini na wanga mwingi unaompatia binadamu nguvu mwilini. Muhogo unaposindikwa vizuri, huweza kutoa unga bora (HQCF) na chips.
- Wakulima wanaweza kuanzisha biashara ndogo ndogo za usindikaji na kujipatia ajira na kupunguza wimbi la watu kuhamia mjini hasa vijana.
- Muhogo uliosindikwa unatupatia bei kubwa zaidi.
- Kiasi cha chakula kinachopotea tangu kuvuna hadi kumfikia mlaji kitapungua
- Usindikaji unapunguza gharama za usafirishaji kwa vile hupunguza ujazo. Hurahisisha udhibiti, upakiaji na upakuaji.
- Utaimarisha bei na kuifanya kutobadilika badilika, hasa wakati wa msimu wa mavuno,
- Usindikaji utaondoa sumu kwenye muhogo
- Usindikaji hupunguza muda wa kuanika muhogo kutoka siku 7-10 (kienyeji) hadi siku 1-2 (ukikereza)
- Unaongezeka ubora kwa kuepuka muhogo kupata uchafu (ontamination) ukilinganisha na njia za kusindika kienyeji ambazo hukaa kwa muda mrefu.
- Muhogo uliosindikwa ni rahisi kuuhifadhi.
- Usindikaji wa kisasa husaidia kupata unga mwingi na bora hivyo kupata nafasi ya kupenya katika soko la ndani na nje.
- Muhogo unaposindikwa hutoa fursa kwa Wakulima wa muhogo kuingia katika teknolojia ya kisasa itakayowasaidia katika uzalishaji wa zao hilo, ikiwa ni pamoja na kuzitumia fursa pekee za mahitaji makubwa ya wanga katika viwanda vya nguo,

vyakula, vinywaji na madawa yanayotenger hapa nchini.

AINA ZA MASHINE ZA KUKEREZA MUHOGO



Mashine ya kukereza muhogo kwa mkono




Kikerezo cha mkono



Mashine zaa kukereza Muhogo kwa mkono



Kikerezo (Manual cassava chippers)



Kukereza kwa mkono



Mashine ya kukereza muhogo kutumia injini ikionyesha sehemu zake. (Chipper)

CASSAVA CHIPPER

VIPIMO:

Ukubwa : 5.5 HP Petrol Engine

Uwezo: 600-800kg/hour

Ulaji wa mafuta : 1.0-1.5 l/hour .

SIFA ZAKE:

Inatoa vipande bora vya kutengeneza unga bora wa muhogo (HQCF) na ni rahisi kuitumia, kubeba na kutengeneza

Kwa Maelezo zaidi wasiliana na:

Katibu Mkuu,
 Wizara ya Kilimo
 S.L.P. 2182
 DODOMA